



# **MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI** **CHUO CHA UFUNDI STADI NA HUDUMA CHA MKOA WA** **DAR ES SALAAM**



## **TANGAZO LA NAFASI ZA MAFUNZO YA UFUNDI WA NGUO NA UBUNIFU** **WA MITINDO YA MAVAZI (TEXTILE AND FASHION DESIGNING)**

Mkuu wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Dar es Salaam anatangaza nafasi za Mafunzo ya Ufundi wa Nguo na Ubunifu wa Mitindo na Mavazi (Textile and Fashion Designing) katika ngazi ya Astashahada (NTA Level 4 Certificate) na Stashahada (Diploma) kwa mwaka wa masomo 2024/2025.

### **1. ASTASHAHADA YA UFUNDI WA NGUO NA UBUNIFU WA MITINDO YA MAVAZI (NTA LEVEL** **4 CERTIFICATE IN TEXTILE AND FASHION DESIGNING) KWA MUDA WA MWAKA MMOJA.**

#### **1.1 SIFA ZA KUJIUNGA**

Mwombaji awe amehitimu Ufundi Stadi Daraja la Tatu (NVA Level 3) na ufaulu usiopungua alama "D" katika masomo yoyote MAWILI ya Kidato cha nne, isipokuwa masomo ya Dini.

**AU**

Mwombaji awe mhitimu wa Kidato cha Nne (Form Four) mwenye ufaulu usiopungua alama "D" NNE isipokuwa masomo ya DINI.

### **2. STASHAHADA YA UFUNDI WA NGUO NA UBUNIFU WA MITINDO YA MAVAZI (DIPLOMA** **IN TEXTILE AND FASHION DESIGNING) KWA MUDA WA MIAKA MIWILI (2)**

#### **2.2 SIFA ZA KUJIUNGA**

Mwombaji awe amehitimu ngazi ya Astashahada ya Ufundi wa Nguo na Ubunifu wa Mitindo ya Mavazi (NTA Level 4 Certificate in Textile and Fashion Designing) Au awe Astashahada katika masomo ya Biashara, Sanaa na Ubunifu, Kilimo, Tehama, Elimu, Sayansi ya jamii au Mwenye sifa zinazoendana kutoka chuo kinachotambulika na Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET)

**AU**

Mwombaji awe amehitimu Kidato cha Sita (Form VI) mwenye ufaulu wa somo moja la Msingi (Principal Pass) na somo moja Tanzu (Subsidiary Pass).

### **3. UTARATIBU NA MUDA WA MAOMBI**

Fomu za maombi ya kozi zinapatikana chuoni (Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha mkoa wa Dar es Salaam - Changómbe) kuanzia tarehe **01/06/2024** kwa gharama ya Shilingi **10,000/=** (Elfu Kumi tu)

**MWISHO WA KUCHUKUA FOMU NI TAREHE 31 JULAI, 2024**  
**MASOMO YATAANZA OKTOBA, 2024**

**KWA MAWASILIANO Z Aid PIGA SIMU: 0787 561 028 AU 0766 693 186**

Imetolewa na  
**Mkuu wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Dar Es Salaam**  
**12 Juni, 2024**